ISHI KWA FURAHA

Imeandikwa Na

S. GHAFFARI

Imetafsiriwa kutoka

Lugha ya Kizungu

Na

ABBAS S. MUSAWI

Chapa ya Mwanzo; 1st June 1971

www.wofis.com *** info@wofis.com

YALIYOMO *Ukurasa*

Maana ya Islamu	1
Mwenye–Enzi–Mungu	2
Koran	3
Mtume Muhammad (s. a. w.)	4
Baada ya Mtume	6
Mafundisho ya Islamu	12
Salaa	15
Saumu	16
Sadaka na Zakaa	16
Hija ya Mecca	17
Mwanamke katika Islamu	18
Ukabila	19
Baadhi ya Methali ya Mtume wa Islamu	22
Baadhi ya Methali ya Ali	24

www.wofis.com *** info@wofis.com

MAANA YA ISLAM

Islam maana yake ni "Kutii amri ya Mwenye-Enzi-Mungu". Dini hii inafundisha unyenyekevu na udugu baina ya watu wote ulimwenguni.

Islam inampa moyo kila mtu kufuata dini yake kwa mujibu wa imani yake bila ya kujali fikra au maoni ya watu wengine hata wazee wake.

Ni rahisi kujifunga na Uislamu. Inahitajia mtu akiri kwa dhati ya moyo wake kuwa:-

1) Hapana Mungu Mwengine ila yule aliyeumba ulimwengu.

2) Muhammad (s.a.w.), ni Mtume wa Islamu na ni mjumbe wa mwisho wa Mwenye-Enzi-Mungu.

3) Ali ni mrithi wa mwanzo (katika warithi 12) wa Mtume Muhammad (s.a.w.) ambaye amechaguliwa na Mtume mwenyewe.

www.wofis.com *** info@wofis.com

Kwa kutamka shahada mbili za mwanzo unakuwa Muislamu. Lakini ukiongezea hiyo shahada ya tatu basi unakuwa Muislamu Shia.

Baadae inafuata kanuni ya Islam na hii inategemea juu ya vitendo vyetu wenyewe. Kanuni hizo ni kama ibada au kazi ya Mwenye-Enzi-Mungu, kazi ya jamii ya watu, kazi ya nchi, biashara, ushirika, harusi, talaka, urithi na kadhalika.

Kwa maelezo kamili mtu lazima asome kanuni ya Islamu ambayo imeandikwa katika karne 14 iliyopita na ambayo inatoa ushahidi kamili juu ya mambo yote.

MWENYE-ENZI-MUNGU

Sheria ya mwanzo na iliyo muhimu kabisa ni kuamini kwa kuwepo Mungu mmoja. Hana mshirika na ni muumbaji wa ulimwengu. Hazai wala hakuzaliwa na hapana kitu cho chote kile kinacho fanana naye.

www.wofis.com *** info@wofis.com

Si muhitaji , hana mfano , haonekani , mwenye nguvu , mjuzi wa kila jambo , mwenye kuishi milele na yupo kila mahala.

Matokeo haiwezi kutengemea kitu kisi - chokuwepo. Hii ina maana ya kuwa matokeo na sababu zake inatosheleza kuonyesha kwa kuwepo mmoja tuu . Kwani wakiwa zaidi ya mmoja , ubishi utaanza juu ya nani ambaye anahusika na matokeo fulani na kwa hivyo ubabaifu utaanza.

KORAN

Koran ni mashairi , mafungu ya maneno na sura zilizotamkwa na Mtume mtukufu wa Islamu , yakiwa ni matamshi na kitabu cha Mwenye-Enzi-Mungu , iliyofumbuliwa kwa Mtume na ambayo alitangaza kuwa ni muujiza wa milele .

Koran inaonyesha maneno ya kweli ya Mwenye-Enzi-Mungu .

Koran tukufu imeleta ushahidi wa ujumbe wake Mtume na Mtume aliwaambia

www.wofis.com *** info@wofis.com

watu wote kuwa hapana mtu atakaeweza kuyaiga au kujaribu kuandika hata kipande kidogo cha Koran.

Koran kama ilivyo sasa ni kitabu kile kile cha Mungu kilichokamilika, bila ya kupunguzwa au kuzidishwa na bila ya kuparaganishwa sura au mashairi. Ni vile vile kama ilivyoandikwa chini ya uangalizi wake mwenyewe Mtume mtukufu.

MTUME MUHAMMAD (S.A.W.)

Muhammad (s. a. w.) alizaliwa Mecca katika mwaka 570 A. D.

Abdullah, baba yake Mtume alifariki dunia kabla ya kuzaliwa kwake Mtume.

Kwa kufuata desturi za aila za watu wa Mecca, Abdul–Muttalib babu yake Mtume, alimpeleka Muhammad (s. a. w) nje ya Mecca na akilelewa na mlezi wake aitwae Halima.

Alipokuwa na umri wa miaka sita, Amena, mama yake (Mtume) alifariki dunia.

www.wofis.com *** info@wofis.com

Na alipofikia umri wa miaka 25, Abutalib, Ammi (baba mdogo) yake (Mtume) alimtaka Muhammad (s. a. w.) ende katika msafara wa biashara wa Khadija, ambaye alikuwa mjane tajiri katika wanawake wa bara ya Arabuni,

Aliporejea kutoka Syria, Khadija alitaka aolewe na Muhammad (s. a. w.) na baadae Mtume alimuowa, akiwa ni mke wake wa mwanzo. Wakati huo Khadija alikuwa na umri wa miaka 40.

Muhammad (s. a. w.) alipata watoto wachache kwa Khadija, lakini wote walifariki dunia katika uhai wake Mtume, isipokuwa Fatimah tu aliyeishi.

Urithi wake (Mtume) ulitokana na mwanawe Fatimah.

Katika umri wa miaka 40 Muhammad (s. a. w.) alipata wahyi (amri) ya mwanzo kutoka kwa Mwenye-Enzi-Mungu na kisha akaanza kutangaza ujumbe wake ulimwenguni.

www.wofis.com *** info@wofis.com

Alipokuwa na umri wa miaka 51, mke wake mtiifu, Khadija, alifariki dunia. Katika uhai wake khadija, Mtume hakuowa mke mwengine.

Katika mwaka 622 A. D. Mtume alihamia Madina.

Baada ya miaka kumi na tatu ya kufundisha na kutangaza dini ya Ulsiamu katika Mecca na miaka kumi na moja katika Madina, Mtume Muhammad (s. a. w.) alifariki dunia akiwa na umri wa miaka 63.

BAADA YA MTUME

Mtume Muhammad (s. a w.) mtaktifu, ambaye alikuwa hatamki kitu ila wahyi kutokana kwa Mwenye-Enzi-Mungu, mara nyingi alinena kuwa watu kumi na mbili katika Ahlul–Bait (aila) yangu waliotajwa na Mungu katika Koran ambao wametakatishwa na Mwenye-Enzi-Mungu mwenyewe (Sura33 Aya33), kuwa mmoja baada ya mwe-

www.wofis.com *** info@wofis.com

ngine ni warithi (Imam) wake Mtume na hao waliochaguliwa ni watukufu, wasiokuwa na dhambi wala makosa na wabingwa katika elimu na wenye huruma kuliko watu wote (isipokuwa Mtume) .

Mrithi wake (Mtume) wa mwanzo alikuwa ni Ali, mtoto wa Abu-Talib.

Ali bin Ammi yake mpenzi Mtume, alizaliwa katika Kaaba (nyumba tukufu ya Mecca). Baada ya kuzaliwa kwake Ali Mtume alimchukuwa na kumlea, na Ali kwa Mtume alikuwa kama mwanawe.

Ali alikuwa mtu wa mwanzo kukubali Uislamu. Kwa mara ya mwanzo, katika miaka miwili baada ya ufumbulio (Wahyi') ya mwanzo, Mtume aliwatangazia watu kuwa "Ali ni mrithi na naibu wangu, msikilizeni na mutii amri yake!"

Ali kwa kujitolea muhanga katika usiku wa kuhama kwake Mtume (kutoka Mecca kwenda Madina), pamoja na usimamizi wake katika vita vyote, ni ushahidi wa kutosholeza

www.wofis.com *** info@wofis.com

yenye mkazo kwa mapenzi yake (Ali), makubwa aliyekuwa nayo juu ya Islamu na Mtume mtukufu.

Ali alimuowa bibi mtakatifu Fatimah, binti wake Mtume Muhammad (s. a. w.). Kutokana kwa Ali na Fatimah walipata watoto wane:-

1- Hassan (Imam wa pili)
2- Husein (Imam wa tatu na Mshujaa wa Karbala)
3- Zainab (Mlinzi wa Islamu katika Koofa na Damascus na alikuwa mke wa Abdullah bin Jaafar). Na
4- Umme - Kulthum (mke wa Ubaidullah bin Jaafar) .

Mbali na matukio rasmi ya tarehe. yapo matangazo mengi ya Mtume ambazo zinaonesha uhusiano pekee baina ya Ali na Mtume. Yafuatayo ni matangazo machache katika hayo aliyoyatangaza Mtume:-

"Mimi na Ali tunatokana katika Nuru

www.wofis.com *** info@wofis.com

moja takatifu."

"E we Ali ! wewe na mimi ni kama Harun na Musa ilivyokuwa hapana Mtume mwengine baada yangu."

"Mimi ni mji wa elimu na Ali ni mlango wake."

"E we Ali ! wewe ni ndugu yangu katika dunia hii na ifuatayo."

"Ali ni ndio Imani yote."

"Ukweli wakati wote utakuwepo pamoja na Ali, na Ali atakuwepo pamoja na ukweli wakati wote."

"Ali yupo pamoja na Koran na Koran ipo pamoja na Ali, hawatogawanyika mpaka watakapofika peponi."

"Mwenye kuhukumu bora (kwa njia ya haki) miongoni mwenu ni Ali."

"Hapana kijana aliyekuwa ni shujaa kuliko Ali."

"Enyi watu ! ye yote yule ambaye mimi ni muongozi wake, basi Ali ni muongozi wake

www.wofis.com *** info@wofis.com

vile vile ".

Na mengi mengineo ambayo mtu anaweza kutafuta katika vitabu vya Ahadith na tarehe .

Hotuba na maneno ya Ali kwa ote pamoja, sasa inaitwa, "Nahjul-Balagha" ambayo ni hazina ya elimu kuu ya ukweli wa Koran na jusuu bora inayoeleza asili ya elimu ya Uislamu. Inasemekana kuwa maneno hayo ni "Chini ya maneno ya Mwenye – Enzi– Mungu na juu ya maneno ya mwanadamu."

Siku ya mwezi 19 Ramadhani (mwezi wa kufunga) 40 A.H; Ali alipokuwa akisujudu katika salaa ya alfajiri, katika msikiti mkuu wa Koofa (Iraq) adui aitwae Abdul-Rahman mtoto wa Muljam alimpiga Ali upanga wa sumu juu ya kichwa chake (Ali), na baada ya siku mbili Ali alifariki dunia. na akazi– kwa katika mji wa Najaf (Al-Ashraf) (Iraq.)

Majina ya Warithi kumi na mbili wa

www.wofis.com *** info@wofis.com

Mtume Munammad (s.a.w.) ambao wamech - aguliwa na Mtume mwenyewe kwa amri ya Mwenye-Enzi-Mungu ni wafuatao :-

Ali (Amirulmuaminin)	Imam	Mtuku	fu wa mwanzo
Hassan-al-Mujtaba	,,	,,	,, pili
Husein(mfalme wa Mashuhadaa)	,,	,,	,, tatu
Ali-al-Sajjad	,,	,,	,, nne
Muhammad-al-Baqer	,,	,,	,, tano
Jaafar-al-Sadeq	,,	,,	,, sita
Musa-al-Kadhim	,,	,,	,, saba
Ali-al-Ridha	,,	,,	,, nane

www.wofis.com *** info@wofis.com

Muhammad- al-Taqi Imam Mtukufu wa tisa
Ali - al - Naqi „ „ „ kumi
Hassan - al - Askariy „ „ „ kumi
na moja
Muhammad - al - Mehdi Imam Mtukufu wa kumi na mbili, wa mwisho, yuhai na ndie anaye subiriwa, adhihiri .

MAFUNDISHO YA ISLAMU

"Hapana utumilivu wa nguvu kuwepo katika dini, kwa hakika ukweli imedhahirisha makosa mojamoja". (Koran 2-256)

Maneno hayo ni ya kuonya kwa uwazi na sio ya kuamuru .

Imeeleza ukweli wa utii wa akili ya binadamu kuwa dini au hali ya utii wa akili na moyo juu ya jambo lo lote lile ikiwa ni la takatifu, haiwezi kupatikana

www.wofis.com *** info@wofis.com

kwa kutumia nguvu, bali kwa kuhakikisha kwa uwazi baina ya utakatifu na uovu.

Baada ya kubainishwa ukweli na uwo-ugo kwa uwazi, akili ya mwanadamu ipo huru kuchagua njia ya haki. Mwanadamu ame-umbwa na akili ili apate kupambanua baina ya ukweli na uwongo na ikiwa mtu ataf-uata njia ya kupotea basi tena hana wa kumlaumu ila ailaumu nafsi yake mwenyewe.

Islam imempa kila mtu madaraka kamili ya kufuata njia ya haki na kila mtu ame-achiliwa kubeba mzigo wake mwenyewe ·

"Wala mtu aliyekuwa na mzigo wake mwenyewe hatoweza kubeba mzigo wa mtu mwengine." (Koran 17-15)

* * * * * * * *

www.wofis.com *** info@wofis.com

Islam inawataka watu wote wenye imani kamili, waheshimu ufumbulio takatifu (wahyi) na waheshimu mafundisho ya wajumbe wote wa kweli wa Mwenye-Enzi-Mungu na wasiwabague miogoni mwao.

Kwa hivyo, Islam inafundisha kumkubali Adam, Nuh, Ibrahim, Musa, Yaqub, Suleiman na Issa kwa kuwa hao in Mitume wa Mwenye-Enzi-Mungu waliyetuletea ujumbe wao na mafumbulio matakatifu ya Mwenye-Enzi-Mungu kwa kila wakati.

Mafundisho ya Watume wote imejengwa juu ya msingi mmoja tu nayo ni "Kutii amri ya Mmwenye-Enzi-Mungu," na wala hapana tafauti katika mafundisho yao ya haki baina ya Watume mbali mbali. Inamkinika kuwa ujumbe uliwahi kugeuzwa kidogo

www.wofis.com *** info@wofis.com

kwa njia nyengine kwa kufuata zama au wakati.

Tunaamini kuwa Muhammad (s.a.w.) ni Mtume wa mwisho na yeye ametufundisha namna ya kuishi kwa ukamilifu, wala tena haitohitajia kuletwa Mtume mwengine.

Mafundisho ya Islamu yanategemea juu ya msingi wa mafumbulio matakatifu, ya Mwenye-Enzi-Mungu na maneno ya Mtume.

SALAA

Salaa ni ukumbusho wa Mwenye-Enzi-Mungu. Katika salaa mtu anafahamu moyoni mwake kwa kuwepo Mwenye-Enzi-Mungu na salaa inamsababisha mtu kuepukana na maovu ya maneno au vitendo. Jukumu la mwanzo na lililo muhimu kabisa katika kazi ya kila Muislamu ni kusali mara tano kila siku.

www.wofis.com *** info@wofis.com

SAUMU (Kufunga Ramadhani)

Mwaka mara moja Waislamu wanatakiwa wafunge mwezi mzima wa Ramadhani, kabla ya kuchomoza jua mpaka jua linapozama. Saumu inasafisha mwili, inaamuru akili na inawatia nguvu moyoni mwa watu wenye imani kufahamu taabu ya kustahamili njaa na kiu zinazowafika mamilioni ya watu waliokuwa masikini duniani na kuwafanya Watoe sadaka na msaada kwa njia ya Mwenye-Enzi-Mungu.

SADAKA NA ZAKAA

Islam inamtaka kila Muislamu atoe pesa kidogo inaotokana katika pato lake na kuipa Beit-ul-Mali ili ipate kuwasaidia masikini na wenye haja.

www.wofis.com *** info@wofis.com

HIJA YA MECCA

Kila Muislamu mwenye uwezo inambidi ende Mecca kuhiji mara moja katika maisha yake. Hii ni safari ya dini na ni mazoezi ya mwili na roho.

Waza, mamilioni ya watu wenye imani ya kweli wanakusanyika Mecca kutoka pembe zote za dunia, kila mwaka mara moja ili kuonyesha imani yao, kukutana na mmoja baada ya mmoja, kuona utukufu wa umoja wa watu wote isiokuwa na kifani na udugu, kwa kusahau lugha zao, rangi ya ngozi, tafauti ya malezi yao na kujiunga katika kundi moja la Waislamu,

Islamu inakataza ubaguzi wa rangi au ukabila. Katika Uislamu, sote ni sawa ikiwa tupo katika pahala pa ibada au pahala pa usawa baina ya watu wote.

www.wofis.com *** info@wofis.com

MWANAMKE KATIKA ISLAM

Islamu ni dini pekee iliyompa mwanamke haki yake katika jumuia ya watu na kumpa haki ya usawa na zile alizopewa mwanamume.

Mwanamke atapewa thawabu kwa mazuri yake na dhambi kwa maovu yake sawa sawa na mwanamume. Jukumu lao kwa Mwenye-Enzi-Mungu ni sawa.

Islamu wakati wote inamuangalia mwanamke kwa uwema na ustahmilivu na kumtendea kwa utukufu na heshima.

Mtume Muhammad (s. a. w.) alisema mara kwa mara kuwa:

" Kusoma elimu ni faradhi ya kila Muislamu (mwanamke, mwanamume, kijana na kizee)."

www.wofis.com *** info@wofis.com

" Pepo ipo chini ya miguu ya mama yenu". (ukimfurahisha mama yako utaingia peponi).

" Ikiwa mume atatumia mapesa kwa ajili ya manufaa ya mke wake, basi hua amemfurahisha Mwenye-Enzi-Mungu na atalipwa kwa mazuri".

Ikiwa mtu (mwanamume) atapata mtoto mwanamke, na kumlea kwa mapenzi bila ya kumuonyesha chuki na kumtendea mazuri yale yale kama anavyomtendea mwanawe mwanamume, basi Mwenye-Enzi-Mungu atamtukuza kwa kumpa pepo"

U K A B I L A

"Enyi watu! kweli tumekuumbeni kuwa ni wanaume na wanawake, na kukuumbeni muwe ni mataifa na makabila ili muweze

www.wofis.com *** info@wofis.com

kutambuana. Kweli yule anaye jilinda na maovu ndie anaye tukuzuwa na Mwenye-Enzi-Mungu. Kweli Mwenye - Enzi - Mungu. ndie mjuuzi wa kila jambo". (Koran 49—13)

Sura hii ya Koran na nyenginezo zinahusiana na udugu wa binadamu. Inaonyesha ukweli kuwa wanaume na wanawake wa kabila au rangi yo yote ile na wanao ishi pahala po pote pale katika sehemu ya dunia wote ni watoto wa wazee wale wale, nao ni Adam na Hawwa.

Sababu ya kugawanyika kwa watu katika mataifa, makabila na majumuia ni kuweza kutambuana.

www.wofis.com *** info@wofis.com

Mtume mtukufu alisema:

" Msichukue fahari kwa uzazi wenu au kwa ukubwa wa makabila na mataifa yenu."

Imam Ali wa nne (Zainul-Abedin) mtoto wa Imam Husein alisema:

" Moto imetengenezwa kwa sababu ya yule mtu asiye mtii Mwenye - Enzi - Mungu hata akiwa ni bwana wa Makurayshi, na pepo imetengenezwa kwa sababu ya yule mtu anaye mtii Mwenye-Enzi-Mungu hata akiwa ni mtumwa mwenye sura mbaya."

Kwa hakika mtu anaweza kupata uhuru wa nafsi, furaha yote, usalama wa roho na maendeleo katika Uislamu tu wala si penginepo.

Islam inaweza kuleta matumainio, raha na uokovu kwa watu wa Afrika, Asia na America na kuwasaidia kupata maisha bora.

www.wofis.com *** info@wofis.com

Katika kupigana na ukabila na ukandamizo, Mwafrica na Mnegro wa America anaweza kutumia Islamu ni kama silaha yake.

Kwa hivyo, juhudi kwa kila upande ifanywe ili Islamu imfike kila mtu ambaye anayepigania haki ya ubinadamu wake.

BAADHI YA METHALI YA MTUME WA ISLAMU

" Tafuta elimu hata ikibidi kwenda China".

" Wino wa mtaalamu ni bora kuliko damu ya Shahidi".

" Kwa hakika mtu hata akitimiza wajibu wake kwa kusali, kufunga, kwenda kuhiji,

www.wofis.com *** info@wofis.com

kutoa sadaka, na kutenda mazuri mengineo, lakini hatolipwa ila kwa kadiri ya fahamu yake".

" Anayefuata njia ya elimu, Mwenye-Enzi-Mungu atamuongoza njia ya peponi".

" Vitendo (maovu) vyako vitarejeshwa kwako kama vile wewe mwenyewe ndie ni muumbaji wa adhabu yako".

" Mlipe mfanya kazi ujira wake kabla ya jasho lake halijakauka".

" Dunia na vitu vyote viliomo ndani yake vina thamani, lakini kitu chenye thamani zaidi kuliko yote ni mwanamke mwenye heshima".

" Ninakuachilieni vitu viwili miongoni mwenu vyenye mizani nazo ni kitabu cha Mwenye-Enzi-Mungu (Koran) na ukoo (Imam 12) wa Ahlul-Bait (aila tukufu ya

www.wofis.com *** info@wofis.com

Mtume) yangu (nao ni, Fatimah, Ali (mume wake Fatimah) na watoto wao Hassan na Husein). Ikiwa mtajiunga na hayo mawili, basi bila ya shaka hamtopotea".

" Ahlul-Bait yangu ni kama Jahazi ya Nuh, ye yote yule ambaye atakaeingia ndani yake basi ameokoka na atakaebakia nje atazama na kupotea".

BAADHI YA METHALI YA ALI

" Mtu amejificha chini ya ulimi wake".

" Mtu asie thamini nafsi yake basi kaangamia".

" Kwa kutomtii Mwenye - Enzi - Mungu, kwa hakika humtii mwanadamu ye yote yule".

www.wofis.com *** info@wofis.com

" Thamani ya mtu intategemea juu ya ustadi aliyoiweza kuipata".

" Usitazame nini anasema, bali sikiliza nini anayoyasema".

" Bora kuwa ni bubu kuliko kusema uwongo".

" Ukweli ulio bora kabisa ni kutimiza ahadi".

" Ye yote anayejijua nafsi yake uzuri, anamjua Bwana Muumbaji wake".

" Mtu mwema ni yule ambaye anaye-wasaidia wenzi wake".

" Vitabu ni bustani ya Mtaalamu".

" Usiwe na haraka ya kutia adabu, bali tafuta njia ya usamehe".

" Ahadi ni deni iliyolipwa kwa kutimiza hiyo ahadi".

" Ujinga ni adui mkubwa anaye chu-kiwa".

www.wofis.com *** info@wofis.com

GROUP OF MUSLIM BROHERS

P. O. Box No. 2245,

TEHRAN. (Iran)

www.wofis.com *** info@wofis.com